**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA**

# TAARIFA KWA UMMA

## WATAHINIWA 11657 KUFANYA MTIHANI WA DARASA LA SABA MANISPAA YA ILEMELA

Tarehe **10** na **11** Mwezi **Septemba 2025**, jumla ya watahiniwa **11657** wa darasa la saba katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela wataungana na wenzao nchini kufanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi.

Kati ya watahiniwa **11657**, wavulana ni **5549** na wasichana ni **6108** wakiwemo watahiniwa **38** wenye mahitaji maalum (**wavulana 21 na wasichana 17).** Aidha watahiniwa wa shule za serikali ni **9402** kati yao wavulana ni **4433** na wasichana ni **4969** na kwa upande wa shule za binafsi watahiniwa ni **2255,** kati yao wavulana ni **116** na wasichana ni **1139.**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, **Bi. Ummy Wayayu**, anatoa rai kwa watahiniwa wote kufuata taratibu na miongozo yote ya mitihani, sambamba na kuwa watulivu huku akiwataka wasijihusishe na vitendo vyovyote vya udanganyifu vitakavyopelekea kufutiwa matokeo yao, Pamoja na hayo anawatakia kila la kheri na kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu awatangulie akiwa na imani kuwa watafanya vyema.

Manispaa ya Ilemela ina jumla ya shule za msingi **134** zenye mikondo **513** kati ya shule hizo shule **80** ni za serikali zenye mikondo **404,** na shule **54** ni za binafsi zikiwa na mikondo **109.**

**Violencea S. Mbakile**
**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali**
**Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela**
**09/09/2025**

**Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, 200 BR.ya Buswelu,33282 Buswelu Ilemela Mwanza, S.L.P 735 BaruaPepe:md@ilemelamc.go.tz, Tovuti: www.ilemelamc.go.tz**